# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)

## MWONGOZO WA UTOAJI HUDUMA ZA UTANGAZAJI KWA NJIA YA WAYA (CABLE)

IMETOLEWA NA TCRA – AGOSTI 2023

# MWONGOZO WA UTOAJI HUDUMA ZA UTANGAZAJI KWA NJIA YA WAYA (CABLE)

Document No: TCRA/EXT/DIA/GUD- CTV/001

| Umeidhinishwa na | Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Dkt. Jabiri K. Bakari | Mkurugenzi Mkuu | [signature] | 22/09/2023 |

## MWONGOZO WA UTOAJI HUDUMA ZA UTANGAZAJI KWA NJIA YA WAYA (CABLE)

### YALIYOMO


SEHEMU YA KWANZA .......... 3

UTANGULIZI .......... 3

1. Jina na kuanza kutumika .......... 3
2. Lengo na Matumizi .......... 3
3. Tafsiri .......... 3

SEHEMU YA PILI .......... 4

UWEZO WA MAMLAKA .......... 4

4. Ukaguzi .......... 4

SEHEMU YA TATU .......... 4

WAJIBU NA MAJUKUMU YA MTOAHUDUMA .......... 4

5. Wajibu wa Msingi .......... 4
6. Ukusanyaji wa Maudhui .......... 4
7. Ubebaji na usambazaji wa Chaneli za Umma .......... 4
8. Kubeba na Kusambaza Matangazo ya Bila kulipia (FTA) .......... 5
9. Umiliki wa Chaneli za Maudhui .......... 5
10. Kumlinda Mteja .......... 5

SEHEMU YA NNE .......... 5

UDHIBITI WA MAUDHUI .......... 5

11. Maudhui yasiyofaa .......... 5
12. Matangazo .......... 6

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

**1. Jina na kuanza kutumika**

Mwongozo huu utanukuliwa kama Mwongozo wa Utoaji Huduma za Utangazaji kwa njia ya Waya (Cable), na utaanza kutumika mara baada ya kupakiwa kwenye tovuti ya Mamlaka.

**2. Lengo na Matumizi**

Mwongozo huu unalenga kuweka msingi wa uendeshaji na usimamizi wa namna ya utoaji wa huduma ya utangazaji kwa njia ya waya. Pia unalenga kutoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utangazaji ili kuleta ufanisi na kuboresha uendeshaji na utoaji wa huduma bora kwa watumiaji na watoa huduma.

**3. Tafsiri**

Katika Mwongozo huu, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Haki Miliki" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi Sura ya 218 ya sharia za Tanzania.

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliyoanzishawa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Sura ya 172 ya Sheria za Tanzania;

"maudhui" maana yake ni taarifa iliyopo katika muundo wa mazungumzo au sauti nyingine, data, maandishi, picha mnato au jongefu, isipokuwa pale ambapo inahusu mawasiliano binafsi;

"Mtoa huduma" Maana yake ni mtu aliyepewa leseni na Mamlaka kubeba na kusambaza maudhui ya Utangazaji kwa njia ya waya;

"mtumiaji" maana yake ni mtu yeyote anayetumia huduma za utangazaji ya televisheni;

"huduma ya maudhui ya chombo cha umma" maana yake ni chombo kinachotoa huduma za utangazaji wa redio, televisheni na kuendeshwa kwa fedha kutoka Serikalini au wafadhili kwa lengo la kutoa mawasiliano mapana hata sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara ikiendesha vipindi kwa ajili ya umma bila kujali faida;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta sura ya 306 ya Sheria za Tanzania;

"Waya" maana yake ni njia itumikayo kupitisha na kusambaza maudhui ya televisheni kwenda kwa watumiaji;

## SEHEMU YA PILI
## UWEZO WA MAMLAKA

### 4. Ukaguzi

4.1 Mamlaka inaweza kufanya ukaguzi kwa Mtoahuduma kwa lengo la kujiridhisha endapo Mtoahuduma anatekeleza matakwa ya Sheria, kanuni na miongozo ya utoaji huduma.

4.2 Mamlaka katika kutekeleza jukumu la ukaguzi, inaweza kushirikisha mamlaka nyingine zinazohusika na utoaji wa huduma za utangazaji kwa njia ya waya.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU NA MAJUKUMU YA MTOAHUDUMA

### 5. Wajibu wa Msingi

Mtoa huduma anatakiwa kuhakikisha anazingatia mambo yafuatayo:

5.1 kujenga na kusimamia miundombinu ya usambazaji wa maudhui kwa njia ya waya;

5.2 kukusanya na kusambaza maudhui ya utangazaji kwa njia ya waya;

5.3 kuwa na mkataba wa utoaji huduma baina yake na: -

i. mtumiaji wa huduma; na,

ii. mmiliki wa maudhui.

5.4 kulipa ada za leseni;

5.5 kuzingatia hakimiliki na haki pekee za wamiliki wengine wa maudhui;

5.6 kuahikisha anakuwa na daftari la wateja ambao wanapewa huduma na kuwasilisha taarifa hizo kwa Mamlaka kwa kila robo mwaka;

5.7 kuweka na kusimamia mfumo wa malipo ya huduma kwa uwazi; na,

5.8 kuweka utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja kwa mujibu wa Kanuni za Ulinzi wa Mteja.

### 6. Ukusanyaji wa Maudhui

Mtoa huduma atakusanya (aggregate) maudhui na kupanga bei kwa kuzingatia Kanuni za Tozo za Huduma (Tariff Regulation GN Na. 22)

### 7. Ubebaji na usambazaji wa Chaneli za Umma

Mtoa huduma atatakiwa kubeba na kusambaza chaneli za utangazaji wa umma kama zitakavyokuwa zimeainishwa na sheria na miongozo mbalimbali bila kutoza malipo kwa watumiaji wa huduma;

## 8. Kubeba na Kusambaza Matangazo ya Bila kulipia (FTA)

8.1 Mtoa huduma ambaye anasambaza huduma za utangazaji kwa njia ya waya atatakiwa kupata kibali toka kwa mtoa huduma za maudhui ya bila kulipia endapo atataka kubeba na kusambaza channeli yake.

8.2 Mtoa huduma atakapotaka kubeba na kusambaza channeli za bila kulipia ataweka mfumo ambao utawezesha watazamaji kupata channeli za bila kulipia hata pale ambapo mtumiaji anapokuwa hajalipa ada husika.

8.3 Bila kuathiri masharti ya haki miliki kwa matangazo, mtoa huduma anaweza kukusanya maudhui ya nje (foreign channels) yanayorushwa na kutazamwa bila kulipia (Free To Air) kutoka kwenye satelaiti.

## 9. Umiliki wa Chaneli za Maudhui

Iwapo mtoa huduma atahitaji kuwa na chaneli ya maudhui ya kulipia (content by subscriprion) au maudhui ya kutazamwa bila kulipia (Free to Air) atapaswa kufuata masharti ya kuomba leseni husika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Leseni.

## 10. Kumlinda Mteja

Ili kumlinda mtumiaji wa huduma za waya, mtoahuduma atahakikisha:

10.1 Anakuwa na mfumo wa kupokea na kushugulikia malalamiko ya wateja;

10.2 Anazingatia ubora wa maudhui ya channeli zinazorushwa ikiwa ni pamoja na uwepo wa picha na sauti zenye ubora; na,

10.3 Ana kuwa na mfumo wa uwazi wa kutoza wateja ambao unajulikana ikiwa ni pamoja na idadi ya vifurushi na bei zake kama mfumo wa kusambaza unaruhusu kufanya hivyo.

# SEHEMU YA NNE
# UDHIBITI WA MAUDHUI

## 11. Maudhui yasiyofaa

Mtoa huduma atahakikisha kuwa chaneli anazobeba na kusambaza zina maudhui yanayozingatia staha, yasiyokiuka mila na desturi, hayachochei uhalifu, au uvunjifu wa amani, yasiyo na viashiria vya vitisho kwa umma, yasiyonyesha ukatili wa watoto, yasiyo na viashiria vya kuingilia faragha za watu wengi au kuvunja utu wa

mwanadamu au makatazo mengine kama yalivyoainishwa kwenye sheria na kanuni nyingine za utangazaji.

**12. Matangazo**

Mtoa huduma hataruhusiwa kuweka tangazo au maandishi yoyote yenye muktadha wa tangazo katika skirini au juu ya chaneli yoyote anayoisambaza kwa watumiaji.

**Dar es Salaam**
**22/09, 2023**

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**